



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA UJENZI NA UCHUKUZI

MAMLAKA YA UDHIBITI USAFIRI ARDHINI



TAARIFA KWA UMMA

KUSITISHA RATIBA ZA MABASI TISA YAENDAYO MIKOANI

YANAYOANZA SAFARI SAA 9.00 ALFAJIRI

Tarehe 19, Juni, 2023

Kwa mujibu wa kifungu cha 5(1)(b) na 6(b) cha Sheria ya Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini Sura ya 413, Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) ina jukumu la kutoa, kuhuisha na kufuta vibali na lesesi za usafirishaji; na **kukuza usalama wa sekta zinazodhibitiwa ikiwa ni pamoja na usalama wa watumiaji wa huduma za sekta zinazodhibitiwa**. Aidha, katika kuhakikisha Mamlaka yetu inatekeleza vyema majukumu yake ya udhibiti katika usafiri wa abiria, Serikali ilitupatia nyenzo (instrument) ya udhibiti wa magari na huduma za usafiri wa abiria - Kanuni za Leseni za Usafirishaji Magari ya Abiria za Mwaka 2020 (Tangazo la Serikali Na. 76 la tarehe 7/2/2020).

Tumekuwa tukipokea taarifa na wenyewe pia kuthibitisha uwepo wa baadhi ya watoa huduma wa mabasi yanayokwenda mikoani kucheza na Mfumo wa Kufuatilia Mwenendo wa Mabasi (*Vehicle Tracking System - VTS*) na kusababisha kusafiri kwa mwendo kasi kwa lengo la kufanya mashindano ya kufika wa kwanza kwenye vituo/stendi za mabasi. Watoa huduma hao wanatumia pia fursa iliyotolewa ya kuanza safari mapema (saa 9 - saa 11 alfajiri) na kufanikisha azma ya kufanya mashindano na kufika wa kwanza kwenye vituo.

Takriban wiki mbili (2) sasa, kumekuwa na taarifa zinazosambaa kwenye mitandao ya kijamii zikionesha mabasi ya *Ally's Star*, *Katarama Express* na *Ismamilo* yakishindana kufika katika vituo vya mabasi. Basi lililoshinda lilimwagiwa maji na kushangiliwa. Hapana shaka, na waliobashiri litawahi, walipata ushindi kwenye Kamari waliyoicheza kinyume na taratibu.

LATRA kwa kuzingatia jukumu lake la **kukuza usalama wa sekta zinazodhibitiwa ikiwa ni pamoja na usalama wa watumiaji wa huduma za sekta zinazodhibitiwa** haiwezi kuacha matendo haya hatari yenye kuhatarisha usalama na maisha ya watu pamoja na mali zichezewa bila kuchukua hatua

stahiki. Kanuni ya 27 (2) ya Kanuni za Leseni za Usafirishaji Magari ya Abiria za Mwaka 2020 inaipa Mamlaka uwezo wa kusitisha leseni ya msafirishaji kwa lengo la kuhakikisha uwepo wa usalama wa usafiri barabarani. Kabla hatujatumia kanuni hii, tunahakikisha tumetoa elimu ya kutosha kwa mto huduma husika. Aidha, baada ya kuona mto huduma hajajirekebisha, tunachukua hatua zingine za kumfanya mto huduma ajirekebishe na kuzingatia Sheria, Kanuni na Taratibu.

Hivyo, kutokana na hali hii na kwa kuwa watoa huduma *Ally's Star* na *Katarama Express* wameendelea kukiuka Sheria, Kanuni na Taratibu hata baada ya kupatiwa elimu na maonyo kadhaa, kwa kuzingatia mamlaka tuliyonayo, tumeputa ratiba zote za **mabasi tisa (9) yanayoanza safari zao kuanzia saa 9.00 alfajiri**. Mabasi hayo ni sita (6) ya *Ally's Star* (T946 EBF, T947 EBF, T948 EBF, T354 DXS, T357 DXS na T360 DXS) na matatu (3) na *Katarama Express* (T835 EBR, T836 EBR, T212 ECR). Mabasi hayo sasa yatapaswa kuanza safari saa 12.00 asubuhi kuanzia **Jumatano, tarehe 21 Juni, 2023**. Endapo wataendelea kukiuka maelekezo haya, tutafuta leseni zao. Tunawashauri wananchi wafahamu haya mabadiliko na kupanga vyema safari zao.

Kampuni ya *Isamilo*, kwa kuwa matukio yake hayajakithiri, pamoja na watoa huduma wengine wanaofanya mchezo huu, tunawapa onyo kali na la mwisho kabla hatujawachukulia hatua stahiki.

Aidha, tunawakumbusha wananchi kutoshabikia vitendo vinavyohatarisha usalama na uhai wa abiria na watumiaji wengine wa barabara. Pia tunawakumbusha madereva na wamiliki kuzingatia Sheria, Kanuni na Taratibu za utoaji huduma za usafiri wa umma. Mamlaka, kwa kushirikiana na Jeshi la Polisi Kikosi cha Usalama Barabarani, tutachukua hatua kali kwa madereva wote watakaobainika kufanya vitendo vinavyokiuka Sheria, Kanuni na Taratibu ikiwa ni pamoja na kuwafutia leseni zao za udereva na kuwafikisha mahakamani kwa hatua zaidi.



CPA Habibu J. S. Suluo
MKURUGENZI MKUU